**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**TAASISI YA ELIMU TANZANIA**

***Dar es Salaam, Tarehe 07 April, 2025***

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Nianze kwa kuwashukuru sana waandishi wa habari kwa kuungana nasi siku ya leo na kwa jitihada zenu endelevu za kuitangaza Tuzo hii ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu tangu ilipoanzishwa katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23 hadi leo.

Kama tunavyofahamu, Tuzo hii ilianzishwa na serikali chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na inaratibiwa na Taasisi ya Elimu Tanzania. Huu ni mwaka wa tatu wa utoaji wa Tuzo hii. Mchakato wa uendeshaji wa Tuzo hii umejumuisha upokeaji wa miswada na usomaji wa miswada hiyo na jopo la majaji. Mchakato huu umeendelea kwa kipindi cha mwaka mzima. Hivi sasa tunaelekea kilele cha utoaji wa Tuzo yenyewe na hafla ya utoaji wa Tuzo hii itafanyika Jumapili tarehe 13 Aprili, 2025 katika Ukumbi wa The Super Dome uliopo Masaki Dar es Salaam.

Tuzo hii kwa Mwaka huu wa 2024 /25 inahusisha nyanja nne za ushairi, riwaya, hadithi za watoto na tamthiliya. Vigezo vilivyotakiwa kutumika katika kushiriki kushindania Tuzo hii vilitangazwa katika vyombo vya habari mbalimbali. Napenda kuwajulisha kuwa mwitikio mwaka huu, kama ilivyokuwa miaka miwili ya nyuma, umekuwa mzuri sana. Watanzania kutoka sehemu mbalimbali za nchi, wanawake kwa wanaume, wameshiriki katika kuwania Tuzo hii.

Ninapenda kuwajulisha kuwa majaji wameshakamilisha kazi ya kusoma miswada iliyopokelewa na orodha teule ya waliopendekezwa kufikiriwa kuwania tuzo hii imekwishapatikana. Hivyo, lengo la taarifa hii ni kutangaza orodha hiyo. Inatarajiwa kuwa washindi wa Tuzo hii watapatikana miongoni mwa orodha hii teule na watatangazwa rasmi siku ya sherehe ya Tuzo. Aidha, ni muhimu kuzingatia kuwa majina katika orodha teule yameorodheshwa kufuatia alphabeti na si kwa kuonyesha nani kashika nafasi gani. Kwa nafasi hii ninaomba kuwatangazia orodha teule kwa nyanja zote nne kama ifuatayo:

**ORODHA TEULE YA WALIOPENDEKEZWA KUFIKIRIWA KUWANIA TUZO YA TAIFA YA MWALIMU NYERERE YA UANDISHI BUNIFU - 2025**

**RIWAYA**

| | **MWANDISHI** | **ANDIKO** | **JINSI** | **MKOA** |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Dkt. Abbas Mohamed Omar | Zawadi ya **S**imu **J**anja | ME | Zanzibar |
| 2 | Ahmad Simba Mwaita | Taifa Jipya | ME | Tanga |
| 3 | George Michael Lauwo | Damu Nzito | ME | Kilimanjaro |
| 4 | Ibrahim Jaffar Mkamba | Mashahidi kutoka Kuzimu | ME | Dar es Salaam |
| 5 | Lucas Gervas Lubango | Bweni la Wavulana | ME | Mwanza |
| 6 | Majaliwa Ibrahim Sued | Kuokoka | ME | Manyara |
| 7 | Maundu Moris Mwingizi | Jeneza la Taifa | ME | Dar es Salaam |
| 8 | Philipo Oyoo Oyaro | Kwa **U**di na **U**vumba | ME | Mwanza |
| 9 | Richard Mziray | Mlezi wa Vizazi | ME | Dar es Salaam |
| 10 | Zakaria Henry Riwa | Kilicho Chetu | ME | Dar es Salaam |

## MKUSANYIKO WA MASHAIRI/UTENZI

| | MWANDISHI | ANDIKO | JINSI | MKOA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Adil Ali Mwinyiae | Yunge | ME | Dodoma |
| 2 | Ally Bakari Mchanyato | Tuzo ya Usomaji | ME | Dar es Salaam |
| 3 | Ally Juma Isuka | Nikifa Msinizike | ME | Dar es Salaam |
| 4 | Bakari Jecha Makame | Diwani ya Tafakuri | ME | Zanzibar |
| 5 | Hussein Kondo Abdallah | Diwani ya Urathi wa Mjumu | ME | Dar es Salaam |
| 6 | Kombo Abdalla Omar | Kisima cha Giningi | ME | Zanzibar |
| 7 | Mbaruku Ally Mohammed | Utenzi wa Nana Mkombozi | ME | Tanga |
| 8 | Peter Gervas Komba | Mashairi ya Maisha | ME | Songea |
| 9 | Saidi Mokiwa Ramadhani | Pendo la Mama Kiboko | ME | Tanga |
| 10 | Sharifa Khamis Mussa, | Pambazuko | KE | Zanzibar |

**HADITHI ZA WATOTO**

| | MWANDISHI | ANDIKO | JINSI | MKOA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Corona Kimaro Cermak | Tembo Zimamoto | KE | Czech Republic |
| 2 | Hafidh Ali Makame | Siafu na Majimoto | ME | Zanzibar |
| 3 | Lilian Simon Mbaga | Hatma Yangu | KE | Dar es Salaam |
| 4 | Mwanacha Mohamed Omar | Mwisho wa Dharau | KE | Zanzibar |
| 5 | Paulina Barnabas Lugabulila | Dirisha la Ajabu | KE | Dar es Salaam |
| 6 | Shifaa Feisal-Amin Ibuni | Maua na **M**ji wa Maweni | KE | Zanzibar |
| 7 | Tune Shaaban Salim | Maziwa Ya Kuku | KE | Dar es Salaam |

**TAMTHILIYA**

| | MWANDISHI | ANDIKO | JINSI | MKOA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ally Nassoro Ngagesa | **Kijarida** | ME | Dar es Salaam |
| 2 | Bupe Anthony Kabute | **Anne na Anelisa** | KE | Dar es Salaam |
| 3 | David Shalali Shaba | **Beti ya Mauti** | ME | Dar es Salaam |
| 4 | Elizabeth Godwin Mahenge | **Pambana** | KE | Dar es Salaam |
| 5 | Faraji Odilo Manoni | **Kovu la Maisha** | ME | Kilimanjaro |
| 6 | Ignas Dennis Mkindi | **Mwale wa Matumaini** | ME | Dar es Salaam |
| 7 | Murungi Raeli Katabarula | **Zaidi ya Majirani** | KE | Kagera |
| 8 | Said Yussuf Kileo | **Mwangaza** | ME | Dar es Salaam |
| 9 | Sajida Salehe Athumani | **Mwangaza wa Mvita** | KE | Dar es Salaam |
| 10 | Tyatawelu Emmanuel Kingu | **Alama ya Kuzaliwa** | KE | Dar es Salaam |

**ZAWADI KWA WASHINDI**
Utaratibu wa zawadi kwa washindi utabaki kama ilivyokuwa miaka iliyopita yaani:

**Mshindi wa kwanza**

Shilingi milioni 10.

Muswada wake utachapishwa na serikali na kusambazwa shuleni na maktaba za taifa.
Ngao
Cheti
**Mshindi wa Pili**
Shilingi milioni 7
Cheti
**Mshindi wa tatu**.
Shilingi milioni 5.
Cheti

Nimalizie kwa kuwashukuru tena kwa kuhudhuria leo na ninawaomba muendelee kuwa pamoja nasi kwa kutusaidia kuitangaza Tuzo hii ili kuwapa nafasi Watanzania kushiriki kwa wingi. Ninatumaini pia kuwa mtahudhuria kwa wingi sherehe ya utoaji wa Tuzo hapo tarehe 13 Aprili 2025. Karibuni sana.

**Imetolewa na:**
**Prof. Penina Oniviel Mlama,**
**Mwenyekiti, Kamati ya Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya uandishi Bunifu.**

**07/04/2025**